

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

Simu: +255 026 23222761-5
Fax No. +255 026 2322624
E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
Mtaa wa Makole
S.L.P. 941,
DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Katibu wa Bunge ambaye ni Msimamizi wa Uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki anautaarifu Umma kwamba, Uchaguzi wa Wajumbe tisa (9) watakwaiwakilisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki utafanywa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa Mkutano wake wa Nane utakaoanza tarehe 13 Septemba, 2022 Dodoma.

Uchaguzi huo unafanyika kwa kuzingatia kuwa maisha ya Bunge la Afrika Mashariki lililoingia madarakani mwaka 2017, yatafikia ukomo wake tarehe 17 Desemba, 2022.

Msimamizi wa Uchaguzi ametoa Tangazo la Uchaguzi huo katika Gazeti la Serikali la leo tarehe 6 Septemba, 2022 kuhusu **Siku ya Uteuzi, ambayo ni tarehe 20 Septemba, 2022, saa kumi kamili jioni, na pia siku ya Uchaguzi ambayo ni tarehe 22 Septemba, 2022 saa tano kamili asubuhi**, mara au mapema baada ya muda wa Maswali, wakati Bunge linaendelea na Shughuli zake.

Kwa Taarifa hii, watu ambao wanazo sifa za kugombea na kuchaguliwa kuwa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki wanaweza kuanza mchakato wa kuteuliwa kuwa wagombea wa nafasi hizo, kupitia Vyama vyao vya Siasa.

Chama au Mgombea aliyeshinda katika ngazi ya Chama anapaswa kujaza **Fomu ya Uteuzi** inayotolewa na Bunge na kuiwasilisha kwa Katibu wa Bunge. Fomu hiyo imetangazwa katika Gazeti la Serikali na inapatikana kwenye Tovuti ya Bunge ambayo ni www.bunge.go.tz.

Imetolewa na:- Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,
Ofisi ya Bunge
Mtaa wa Makole
41105 DODOMA.

6 Septemba, 2022